KISWAHILI · SWAHILI

# Nyenzo kwa ajili ya Jamii Jimbo la New York

Mwongozo wa Rasilimali na Taarifa
kwa wahamiaji New York
Julai 2026




**New York Immigration Coalition**
nyic.org

Shirikisho la Wahamiaji New York wameandaa nyenzo hii ili kuwasaidia wanajamii, wadau wetu na wanaofanya kazi pamoja nao. Nyenzo hii inaboreshwa mara kwa mara kwa kutegemeana na mabadiliko ya sera na sheria.

Taarifa ilisasishwa mara ya mwisho: 7.31.2026

## Yaliyomo


- Hadhari ya Jamii **3**
- Fahamu Hako Zako **6**
- Afya **10**
- Shule na elimu **13**
- Usalama wa Jamii **16**
- Taarifa zinazopatikana NYS **17**

# Hadhari ya Jamii

## Kuondolewa Nchini Kwa Mchakato wa Haraka

### Trump Anapanua Mchakato wa "Expedited Removal" ili Kuwaondoa Wahamiaji Nchini Kwa Haraka

- Mahakama ya serikali ya shirikisho imeruhusu Utawala wa Trump kupanua mchakato wa "expedited removal" ili kuwaondoa wahamiaji nchini bila ya kuonekana mbele ya hakimu wa uhamiaji.
- Marekani sehemu yoyote, inawezekana sasa kwamba wahamiaji wasio na vibali na wasioweza kuhakikisha kwamba wamekuwepo nchini kwa angalau miaka miwili wataweza kuondolewa nchini kwa mchakato wa harkaka.

### Nani yumo hatarini zaidi?

- Ikiwa miaka miwili bado haijapita tangu ulipoifika Marekani, unaweza kuwa kwenye hatari ya kuondolewa nchini kwa mchakato wa haraka. Mchakato huu unaitwa "expedited removal."
- Unaweza kuwa kwenye hatari ikiwa:
  - Miaka miwili bado haijapita tangu ulipoifika Marekani, na
  - Uliingia Marekani bila kufanyiwa ukaguzi (maana ulivuka mpakani katikati ya sehemu rasmi za kuingia), uliingia Marekani kupitia programu ya msamaha (parole) mfano CHNV parole, au uliingi Marekani kupitia kitumizi (app) cha CBP One.

### Vipa naweza kujilinda?

- Ikiwa umekuwepo Marekani kwa zaidi kuliko miaka miwili, unashauriwa kubeba ushahidi wa kuwepo kwako nchini, mfano nakala nzito za mkataba wa kupangisha nyumba au bili za umeme zinazohusika na kipindi hicho ambacho umekaa nchini.
- Tunza nakala za ushahidi wako wa kuwepo nchini nyumbani kwako na/au kwa mtu mwaminifu kwako mfano rafiki, mwanafamilia, au mwanasheria.
- Ikiwa unastahilika, uhakikishe kwamba umefaili ombi lako la hifadhi au maombi mengine kwa Mahakama ya Uhamiaji au Ofisi ya Huduma za Uraia na Uhamiaji wa Marekani (USCIS), na ubebe mwilini ushahidi wa maombi ambayo umeshayawasilisha.
- Unaweza kuipigia simu Ofisi ya Wamarekani Wapya ya Jimbo la New York katika namba yake maalumu ya 1-800-566-7636, kuuliza maswali na kupata mapendekezo ya wapi pa kupata ushauri wa kisheria kuhusu mambo ya uhamiaji.

### Vipi naweza kujiandaa kwa uwezekano wa kuwekwa kizuizini?

- Kuwa tayari na kuwa na mpango wa usalama pamoja na familia yako na wanajamii wenzako ikiwa mmojawenu anawekwa kizuizini.
- Uunganishwe na vikundi vya msaada wa mahakama, au uwe na mtu wa kukusindikiza mahakamani na kwenye miadi zako na Wizara ya Usalama wa Ndani (DHS).
- Ikiwa unawekwa kizuizini na unaogopa kurudishwa nchini kwako na/au kupelekwa nchini kengine, sema hii wazi kwa maafisa wa ICE na kwa maafisa wengine wowote wa uhamiaji. Inawezekana kwamba utahitaji kusema hii mara kadhaa. Hata kama umeshatuma ombi lako la hifadhi, ueleze mara nyingine hofu yako ya mateso na unyanyasaji.

# Hadhari ya Jamii

## Kukomeshwa kwa TPS

### Maamuzi ya Mahakama Kuu yanakomesha hali ya TPS kwa Wahaiti na Wasiria

- Juni 25, 2026, Mahakama Kuu ya Marekani ilitoa amri inayoiruhusu Utawala wa Trump kukomesha uteuzi wa Hali ya Kulindwa Kwa Muda (Temporary Protected Status [TPS]) kwa Haiti na Siria.
- Zaidi kuliko wakazi 40,000 wa New York watapoteza kinga ya kisheria hivi karibuni, na watakuwa kwenye hatari ya kuwekwa kizuizini na kuondolewa nchini. Maamuzi haya pia yanasaidia Utawala wa Trump ikiwa unataka kukomesha uteuzi wa TPS kwa nchi zingine siku za usoni.

### Hii inamaanisha nini na kipi kitafuata?

- Wahaiti na Wasiria wenye TPS hivi karibuni watapoteza uwezo wao wa kukaa na kufanya kazi Marekani kihalali.
- Amri ya Mahakama Kuu inapangwa kuwa sheria kuanzia Julai 27, 2026, isipokuwa hakuna amri zingine za mahakama. Wizara ya Usalama wa Ndani (DHS) inatarijiwa kufanya matendo zaidi hivi karibuni ili kukomesha hali ya TPS kwa Haiti na Siria. Fuata uscis.gov/TPS kwa taarifa zaidi.
- Ikiwa unaathirika na maamuzi haya, usishikwe na hofu. Fanya matendo sasa kujilinda wewe na kulinda familia yako.

### Vipi naweza kujilinda?

- Ikiwa unayo hali ya TPS sasa hivi:
  - Uongee na mwanasheria wa uhamiaji anayeaminiwa au mwakilishi anayetambuliwa rasmi karibuni iwezekanavyo ili ugudue unayo machaguo gani? Hutokea mara nyingi wenye hali ya TPS wana njia zingine za kupata hali ya uhamiaji, zikiwemo njia kupitia familia na uajiri.
    - Kuwa mwangalifu kuhusu utapeli, wanasheria feki, na mtu yeyote yule anayeahidi kwamba, bila shaka yoyote, utapata manufaa ya uhamiaji.
  - Usiondoke Marekani bila ya ushauri wa kisheria. Ikiwa unaamua kuondoka, inawezekana kwamba maombi ya uhamiaji ambayo umeshayawasilisha yatadhaniwa kuachwa, na ungeweza kuzuiwa kurudi Marekani siku za usoni.
  - Kuwa tayari na kuwa na mpango wa usalama pamoja na familia yako na wanajamii wenzako ikiwa unawekwa kizuizini.
  - Fahamu Haki Zako! Ikiwa maafisa wa ICE wanakuja kukutafuta, una haki ya kunyamaza kimya. Unaweza kuwakataa wasiingie nyumbani kwako ikiwa hawana hati ya mahakama.
  - Ikiwa maafisa wa ICE wanakukamata, uwaambie mara moja kwamba unaogopa kurudi nchini kwako ulipozaliwa na/au kupelekwa nchini kengine. Inawezekana kwamba utahitaji kusema tena kwa maafisa wa uhamiaji kwamba unataka kupewa mahojiano ya hofu inayoaminika, na fursa ya kuomba hali ya hifadhi.

### Rasilimali

- Kupata taarifa na rufaa za msaada wa kisheria, uipigie simu Ofisi ya Wamarekani Wapya ya Jimbo la New York katika 1-800-566-7636
- Wakazi wa Jiji la New York wanaweza pia kuipigia simu MOIA Immigration Legal Support Hotline katika 1-800-354-0365, au kupiga 311 na kusema “Immigration Legal”
- Tembelea www.immigrationadvocates.org/legaldirectory kupata orodha ya mashirika yanayotoa huduma za kisheria kuhusu uhamiaji, kwa bure au kwa bei nafuu, katika sehemu mbalimbali nchini

# Hadhari ya Jamii

## Usikilizaji wa Kalenda aina ya Mega Master

### Mahakama za Uhamiaji Zinapanga Usikilizaji wa Kalenda aina ya "Mega Master"

- "Usikilizaji wa kalenda aina ya mega master" ni usikilizaji wa kesi unaopangwa kwa watu mia au zaidi katika wakati mmoja, kwa kulenga hasa watu wasio na wanasheria wa kuwawakilisha. Kwa wahamiaji wengi, usikilizaji wa kalenda aina ya master ni mara yao ya kwanza mbele ya hakimu katika kesi zao za uhamiaji.
- Ikiwa umeshapangiwa tarehe ya usikilizaji, inawezekana kwamba tarehe itasogezwa mbele.

### Nini itatokea nikikosa tarehe yangu ya kwenda mahakamani?

- Kwa baadhi ya watu, tarehe zao za usikilizaji zinasogezwa mbele, na inawezekana kwamba watakosa tarehe zao kwa sababu hawajui kwamba tarehe zimebadilishwa.
- Ikiwa unakosa usikilizaji wako wa kalenda aina ya master, utapewa amri ya kuondolewa. Hii inamaanisha kwamba utaweza kuwekwa kizuizini na/au kuondolewa nchini.

### Vipi naweza kuhakikisha kwamba najua tarehe yangu ya kwenda katika mahakama ya uhamiaji?

- Ikiwa una kesi katika mahakama ya uhamiaji, itabidi uangalie tovuti ya mfumo wa taarifa za kesi inayojiendesha yenyewe (EOIR automated case information system website), au piga simu mara kwa mara kujifunza kama kuna mabadiliko yoyote ya tarehe za usikilizaji.
- Kuhakikisha tarehe na mahali pako pa kwenda mahakamani:
  - Tembelea acis.eoir.justice.gov na kuingiza namba yako ya "A" ya tarakimu tisa (9-digit A-number), au
  - Piga 1-800-898-7180 na fuata maelekezo.

### Vipi naweza kujilinda?

- Uhakikishe tarehe yako ya kwenda mahakmani mara kwa mara ili usikose usikilizaji wako wa kesi.
- Uwe tayari na kufanya mpango wa usalama pamoja na familia na wanajamii ikiwa inatokea kwamba unawekwa kizuizini.
- Uunganishwe na vikundi vya msaada wa mahakama, au uwe na mtu wa kukusindikiza mahakamani kwa ajili ya usikilizaji wako.
- Ikiwa unastahilika, uhakikishe kwamba umefaili ombi lako la hifadhi au maombi mengine kwa mahakama.
- Ikiwa unawekwa kizuizini na unaogopa kurudishwa nchini kwako na/au kupelekwa nchini kengine, sema hii wazi kwa maafisa wa ICE na kwa maafisa wengine wowote wa uhamiaji.
- Unaweza pia kuipigia simu Ofisi ya Wamarekani Wapya ya Jimbo la New York katika namba yake maalumu ya 1-800-566-7636, kuuliza maswali na kupata mapendekezo ya wapi pa kupata ushauri wa kisheria kuhusu mambo ya uhamiaji.

### Fahamu Haki Zako Mahakamani

- Una haki ya kupinga ufutaji wa kesi yako au kuondolewa kwako nchini kabla hakimu hajafanya maamuzi.
- Unaweza kudai kwamba mwanasheria wa ICE awasilishe ombi lake la kufuta kesi au kukuondoa nchini kwa maandiko, ili uwe na muda wa kumweleza hakimu kwa nini unataka kuendelea na kesi yako na kutafuta msaada wa kisheria.
- Ikiwa hakimu anafuta kesi yako au kuamuru unondolewe, una haki ya kukata rufaa. Unaweza kukata rufaa maamuzi hayo kwa Bodi ya Kukata Rufaa za Uhamiaji (Board of Immigration Appeals [BIA]). Uhakikishe kwamba umwambie hakimu wa uhamiaji kwamba unataka kukata rufaa.
- Kwa rasilimali zaidi kuhusu haki zako, tembelea nyic.org/kyr

# Fahamu Hako Zako

## Utekelezaji wa Uhamiaji

### Nini inatokea?

- Chini ya Rais Trump, kumekuwa na ongezeko la utekelezaji wa uhamiaji katika jamii zetu.
- Maafisa wa Idara ya Uhamiaji na Utekelezaji wa Forodha (Immigration and Customs Enforcement [ICE]) na Ofisi ya Udhibiti wa Forodha na Mipaka (Customs and Border Patrol [CBP]) wameongeza kiasi cha uvamizi wa uhamiaji na kukamatwa kwa watu. Mara nyingi hushirikiana na vyombo vingine vya sheria kama mapolisi na masherifu. Kutokana na haya, tumeona wanajamii wengi zaidi ambao wamefungwa katika vituo vya kizuizini na kuwekwa kwenye mchakato wa kuondoloewa.
- Watu waliofika Marekani hivi karibuni, watu wasio na vibali, watu wasioongea Kiingereza kama lugha yao ya kwanza, na watu wengine wako kwenye hatari ya utekelezaji wa uhamiaji.
- Ushauriane na mwanasheria wa uhamiaji ikiwa una wasiwasi.

### Je, nina haki gani ikiwa ninasimamishwa na maafisa wa ICE au CBP?

- Ni muhimu ufahamu haki zako wakati wowote unakutana na maafisa wa Idara ya Uhamiaji na Utekelezaji wa Forodha (ICE), Ofisi ya Udhibiti wa Forodha na Mipaka (CBP), au vyombo vingine vya sheria.
- Ikiwa unasimamishwa na maafisa wa uhamiaji au chombo kingine cha sheria, ukumbuke:
  - Tulia. Usikimbie. Usimpinge au kumzuia afisa.
  - Usiseme uongo au kutoa hati bandia.
  - Una haki ya kunyamaza kimya na kutokujibu maswali. Unaweza kusema, "I want to remain silent" ("Nataka ninyamaze") or "I don't want to answer questions" ("Sitaki kujibu maswali".
  - Ikiwa afisa anauliza kama anaweza kukupekua au kupekua mali zako, una haki ya kusema hapana. Unaweza kusema, "I do not consent to a search" ("Sitoi ruhusa kupekuliwa").
  - Una haki ya kujua kama na kwa nini unawekwa kizuizini au kukamatwa. Unaweza kuuliza, "Am I free to go?" ("Niko huru kuondoka?") au "Why am I being detained?" ("Kwa nini ninawekwa kizuizini?").
  - Una haki ya kurekodi kinachokutokea na kinachowatokea watu wengine. Unaweza kusema, "I have a right to record" ("Nina haki ya kurekodi").
  - Ikiwa unasimamishwa, kuwekwa kizuzini, au kunyanyaswa na maafisa wa utekelezaji wa sheria, jaribu kupata majina na namba za beji za maafisa, pamoja na taarifa zozote zingine za kuwatambulisha.
- Kwa rasimali za "Fahamu Haki Zako" (Know Your Rights [KYR]) katika lugha mbalimbali, tembelea nyic.org/kyr

### Je, nina haki zingine za ziada ikiwa maafisa wa ICE au CBP wanakuja nyumbani kwangu au mahali pangu pa kazi?

- Nyumbani kwako na maeneo mengine ya faragha, yaani "private spaces" (mfano maeneo yoyote ya mahali pa kazi ambayo wanaruhusiwa kuwepo waajiriwa tu) yana ulinzi maalumu ambao maeneo ya umma hayana.
- Maafisa wanaweza kuingia maeneo ya faragha ikiwa tu wana ruhusa yako au wakikuonesha hati ya mahakama inayosainiwa na hakimu.
- Ikiwa maafisa wa ICE wanakuja nyumbani kwako, unaweza kutokufungua mlango au kusema, "I do not consent to a search" ("Sitoi ruhusa kupekuliwa") na kuuliza kuona hati ya mahakama.

### Rasilimali

**Know Your Rights Wallet Card:**

**Know Your Rights Curriculum:**

**Know Your Rights with CBP:**

**Immigration Enforcement at the Workplace:**

# Fahamu Hako Zako

## Immigration Enforcement

### Je, naweza kufanya nini ikiwa ninaona maafisa wa ICE au CBP wakiwa wanawakamata watu au kufanya uvamizi wa uhamiaji?

- Ikiwa unaona maafisa wa ICE au CBP wakiwa wanawakamata watu, tulia na kumbuka haki zako.
- Uzingatie mavazi na magari ya maafisa, na maneno na alama zozote zikiwepo.
- Ikiwa unajisikia salama, chukua video au piga picha za kinachoendelea. Unaweza pia kuandika habari yote ya kinachotokea.
  - Uwe salama. Usiingilie na maafisa.
- Ikiwa inafaa, ushirikishe taarifa kuhusu shughuli za utekelezaji ndani ya mitandao yako ya watu inayoaminika. Sehemu nyingi zina namba za simu maalumu unapoweza kupiga ili kuripoti utekelezaji wa uhamiaji.
- Uhakikishe kwamba ushirikishe tu taarifa zilizothibitishwa: kitu ulichoshuhudia wewe mwenyewe au alichoshuhudia mtu unayemwamini. Ukumbuke: ukweli, si woga!
- Uwasaidie watu na familia zilizoathirika. Ikiwa mtu anawekwa kizuizini au kukamatwa, ushirikiane na vikundi vya kijamii vinavyoaminika kuwasaidia familia yake na wapendwa wake. .
- Tafuta ushauri kwa mwanasheria wa uhamiaji anayeaminiwa.
- Kwa rasilimali kuhusu nini cha kufanya ikiwa unawaona maafisa wa ICE au CBP, tembelea nyic.org/kyr na kutafuta makala jina lake “If You See Immigration Enforcement.”

### Je, vipi naweza kujiandaa kwa uwezekano wa kuwekwa kizuizini mimi kwangu au kwa jamaa yangu?

- Ikiwa wewe si raia wa Marekani na una watoto, uwe na mpango iktokea unawekwa kizuizini na afisa wa ICE, CBP au wakala nyingine.
- Ili kuwa tayari, itabidi ufanye hivi:
  - Tunza vizuri nyaraka muhimu. Uziweke mahali ambapo wanafamilia wengine wataweza kuzipata kama watahitaji.
  - Amua ni nani ambaye ungetaka kuwatunza watoto wako usingeweza kufanya mwenyewe.
  - Umteue kisheria mtu awe mlezi wa watoto wako.
    - Njia mbili kuu za kumteua kisheria mtu awe mlezi ni:
      - Uteuzi wa Mtu katika Uhusiano wa Mzazi (Designation of Person in Parental Relationship)
      - Uteuzi wa Mtu wa Kuwa Mlezi Ikitokea Dharura (Standby Guardianship)
  - Jaza fomu za ziada kwa ajili ya mtoto wako, ikiwemo Travel Authorization Form au School Emergency Contact Form
  - Unaweza kufikiria pia kujaza fomu ya Power of Attorney
- Kwa taarifa zaidi, tembelea nyic.org/kyr na tafuta kipengele cha “Family Preparedness” (Kuwa Tayari Kama Familia).

### Rasilimali

**If You See Immigration Enforcement:**

**Family Preparedness Guide:**

**Family Preparedness Forms:**

# Fahamu Hako Zako

## Immigration Detention

### Ikiwa ninawekwa kizuizini, ninazo haki gani?

- Ukumbuke, una haki, hata ukiwa kizuizini!
    - Una haki ya kunyamaza kimya na kutokujibu maswali.
    - Una haki ya kuongea na mwanasheria, au kuchukua muda wa kumtafuta mwanasheria.
    - Una haki ya kutembelewa na mwanasheria huko kizuizini.
    - Una haki ya kupiga simu. Unaweza kumpigia simu mwanasheria au familia yako.
    - Una haki ya kuwasiliana na ubalozi wako.
    - Huhitaji kusaini kitu chochote.

### Vipi naweza kugundua mtu aliyewekwa kizuizini yupo wapi?

- Kumtafuta mtu ambaye yuko kizuizini kwa ICE sasa hivi:
    - Nenda locator.ice.gov na ingiza taarifa zifuatazo:
        - Jina, nchi ya kuzaliwa, na tarehe ya kuzaliwa, au
        - Namba ya “A” (A-number) ya tarakimu tisa
    - Kifaa cha ICE cha kutambua mahali (locator) kinapaswa kuonesha mahali anapowekwa kizuizini mtu mhusika. Lakini inaweza kuchukua muda kabla mtu mhusika hajaonekeana kwenye mfumo.
    - Ukidhani kwamba ndugu yako mpendwa yuko kizuizini kwenye kituo mahususi cha ICE, unaweza pia kumtafuta kupitia:
        - Kumtafuta katika accesscorrections.com. Jina lake likionekana, kuna uwezekano mkubwa kwamba yuko kizuizini kwenye kituo hicho ulichochagua.
        - Kuwasiliana na kituo fulani moja kwa moja kupitia ice.gov/detention-facilities
    - Ikiwa huwezi kumpata mtu mhusika kwa kutumia mifumo hii ya mtandao, unaweza kuwasiliana na ofisi ya ICE aina ya Nyendo za Utekelezaji na Ufukuzaji (Enforcement and Removal Operations [ERO]): ice.gov/contact/field-offices
    - Kwa taarifa zaidi kuhusu kumtafuta mtu ambaye amekamatwa au kuwekwa kizuizini kwa wahamiaji, tembelea nilc.org/resources/how-to-find-a-loved-one-after-a-u-s-immigration-arrest/
        - Rasilimali hii inapatikana katika lugha 9, zikiwemo Kiingereza, Kiarabu, Kichina, Krioli ya Haiti, Kikorea, Kitagalog, Kivietnam na Kihispania.

### Wasiliana na watu ukiwa kizuizini?

- Unaweza kupiga simu namba maalumu kwa watu wahamiaji wanaowekwa kizuizini ili upate taarifa zaidi pamoja na rasilimali.
- Kupiga simu Namba Maalumu ya Kitaifa ya Utetezi wa Wahamiaji, piga 9233# kutoka kwa simu ya mahali ambapo umewekwa kizuizini. Namba maalumu hiyo ni bure, mazungumzo hayasikilikzwi, na huduma zinapatikana Jumatatu hadi Ijumaa, kuanzia saa tano asubuhi hadi saa tano usiku (11am-11pm).
- Kupiga simu namba maalumu ya Haki kwa Familia za Wahamiaji (Justice for Migrant Families), inayopatikana kwa wanaowekwa kizuizini Kituo cha Serikali ya Shirikisho cha Buffalo (Buffalo Federal Detention Facility), piga 716-427-4917, Jumatatu hadi Alhamisi, kuanzia saa nane mchana hadi saa kumi mchana (2pm-4pm) na kuanzia saa kumi na mbili jioni hadi saa mbili usiku (6pm-8pm).

### Rasilimali

**Immigration Detention Support:**

**NILC’s Guide “How to Find a Loved One after a U.S. Immigration Arrest”:**

# Fahamu Hako Zako

## Mahakama ya Uhamiaji

### Vipi naweza kugundua kama nina usikilizaji wa kesi yangu ya uhamiaji, pamoja na tarehe na muda uliopangwa?

- Kutafuta tarehe ya kwenda mahakamani, pamoja na mahali:
  - Tembelea acis.eoir.justice.gov na kuingiza namba ya "A" ya tarakimu tisa, au
  - Piga simu 1-800-898-7180 na fuata maelekezo.

### Wapi naweza kupata msaada wa kisheria?

- Kupata taarifa na rufaa za msaada wa kisheria, uipigie simu Ofisi ya Wamerikani Wapya ya Jimbo la New York katika 1-800-566-7636.
- Wakazi wa Jiji la New York wanaweza pia kuipigia simu MOIA Immigration Legal Support Hotline katika 1-800-354-0365, au kupiga 311 na kusema "Immigration Legal"
- Tembelea www.immigrationadvocates.org/legaldirectory kupata orodha ya mashirika yanayotoa huduma za kisheria kuhusu uhamiaji, kwa bure au kwa bei nafuu, katika sehemu mbalimbali nchini
- Jihadhari na utapeli unaowalenga wahamiaji.
  - Sheria ya uhamiaji ni changamano, ina mambo mengi. Uwe mwangalifu wakati wa kuzungumzia suala lako na mtu au biashara yoyote.
  - Uzungumze na mwanasheria tu au mwakilishi anayetambuliwa rasmi wa Wizara ya Haki (Department of Justice [DOJ]) kwa ushauri wa kisheria kuhusu suala lako.

### Vipi naweza kumsaidia mtu anayeachiwa huru kutoka kizuizini?

- Dhamana ni hela inayolipwa DHS kudhamini kwamba, mtu mhusika akiachiwa huru, ataonekana mahakamani kwa usikilazaji mara zote anapopaswa kuonekana.
- Ikiwa ndugu yako mpendwa amepewa dhamana asiyoiweza, inawezekana kwamba anaweza kupata msaada kutoka kwa mfuko fulani wa kulipia dhamana.
- Kwa taarifa kuhusu dhamana katika jimbo la New York, tembelea envisionfreedom.org/get-support
- Kwa orodha ya mifuko maalumu ya kulipia dhamana katika sehemu mbalimbali nchini, tembelea bit.ly/localbailfunds

### Rasilimali

**EOIR Automated Case Information for Immigration Court:**

**Immigrant Advocates Network Legal Directory:**

**Envision Freedom's bond/ post-release resources:**

# Afya

## Pata bima ya afya

### Bima ya afya ni nini na nani anastahilika?

- Bima ya afya inasaidia kulipia huduma za afya, mfano kuonana na madaktari, kulazwa hospitali, maagizo ya matumizi ya dawa, na huduma za dharura. Inaweza kupunguza gharama za huduma za afya, na kusaidia kukulinda kutoka bili kubwa za huduma za afya.
- Watu wengi wanastahilika bima ya afya. Inawezekana kwamba unakidhi vigezo vya mipango mbalimbali kutokana na kazi yako, mapato, umri, ulemavu, hali ya uhamiaji, n.k.
- Kuona ukikidhi vigezo vya kupata bima ya afya, tembelea: nystateofhealth.ny.gov

### Je, wahamiaji wasio na vibali wanastahilika bima ya afya?

- Inawezekana kwamba unastahilika bima ya afya kutokana na umri wako na/au mapato.
- Wahamiaji wasio na vibali wanaoishi katika Jimbo la New York, kuwa na umri wa miaka 65 au zaidi, na kukidhi vigezo fulani vya mapato, wanastahilika Medicaid.
- Watoto wasio na vibali wenye umri wa chini ya miaka 19 wanastahilika mpango wa Child Health Plus (CHP), ambao unatoa mafao ya bima ya afya kwa bure au kwa bei ndogo, bila kujali mapato wala hali ya uhamiaji.

### Vipi najiandikisha kwa bima ya afya?

- Wakazi wa New York wanaweza kupata bima ya afya ya umma na bima ya afya ya kampuni binafsi kupitia NY State of Health.
  - Ukikidhi vigezo vya kuwa na Medicaid, Essential Plan au Child Health Plus, kipindi cha kujiandikisha kiko wazi mwaka mzima.
  - Ukipata bima ya afya ya kampuni binafsi kupitia soko la mtandao la ACA (marketplace), kipindi cha kujiandikisha ni kuanzia Novemba 1, 2026 - Desemba 15, 2026; kipindi hiki ni kifupi zaidi kuliko vipindi vya miaka ya nyuma.
    - Ikiwa unakidhi vigezo vya Kipindi Maalumu cha Kujiandiksha (Special Enrollemnt Period), kwa sababu kama mabadiliko ya hali ya uhamiaji, mapato, n.k., inawezekana kwamba utaweza kujiandiksha nje ya kipindi cha kawaida cha kujiandikisha.
- Jinsi ya Kujiandikisha
  - Pata msaada wa bure wakati wa kujiandikisha kutoka kwa Navigator, ana kwa ana au kupitia simu. Tafuta Navigator hapa: info.nystateofhealth.ny.gov/ipanavigatorsitelocations
  - Pigia simu Kituo cha Kuwahudumia Wateja cha NY State of Health 1-855-355-5777 (TTY: 1-800-662-1220).
  - Mtandaoni katika nystateofhealth.ny.gov. Kipengele cha ku-chat kinapatikana kwenye tovuti wakati wa masaa ya biashara kwa ajili ya kukusaidia kukamilisha fomu yako ya maombi.
  - Wakazi wa New York City: piga 311, tuma SMS inayosema "CoveredNYC" kwenda 877-877, au tembelea on.nyc.gov/healthinsurance kwa msaada na taarifa zaidi.
- Pata taarifa kuhusu mafao ya bima ya afya kwa lugha mbalimbali hapa: info.nystateofhealth.ny.gov/InformationalMaterials

### Rasilimali

**New York State of Health Website:**

**NYS Health Multilingual Resources:**

# Afya

## Pata huduma za afya

### Je, huduma za afya zinapatikana kwa watu wasio na bima ya afya?

- Hata kama hujakidhi vigezo vya kupata bima, bado unaweza kupokea huduma za afya za dharura. Inawezekana pia kwamba utaweza kupata huduma za afya katika vituo vya afya vya kijamii, vituo vya afya vingine, na kupitia programu za afya za mitaa.
- Vituo vya afya vinavyostahilika kwa msaada wa serikali ya shirikisho (Federally qualified health centers [FQHCs]) lazima vitoe huduma za afya bila kujali uwezo wa mtu kulipa, au kutokuwa na bima ya afya. Vinagharamisha kadiri unavyoweza kulipa kwa mujibu ya mapato yako, na haviulizi ushahidi wa hali ya uhamiaji.
    - Kupata kituo cha afya kinachostahilika kwa msaada wa serikali ya shirikisho cha hapo karibu, tembelea findahealthcenter.hrsa.gov
- Vilevile kuna huduma fulani za afya unazoweza kuzipata bila ya bima ya afya.
    - Vipimo vya Kansa/Saratani:
        - Ikiwa huna bima ya afya, Jimbo la New York linatoa vipimo vya kansa/saratani vya bure kwa kansa/saratani ya matiti, shingo ya kizazi, na utumbo mpana na rektamu.
        - Kwa taarifa zaidi, tembelea health.ny.gov/diseases/cancer/services
- Chanjo:
    - Ikiwa huna bima ya afya, programu ya Jimbo la New York ya Chanjo kwa Watu Wazima (Vaccines for Adults [VFA]) inawatolea chanjo za bure kwa watu wazima wanaostahilika. Chanjo zinasambaziwa vituo vya afya vinavyoandikishwa kama watoaji kupitia hiyo programu ya VFA.
    - Kwa taarifa zaidi, tembelea health.ny.gov/prevention/immunization
    - Kwa orodha ya chanjo zinazopendekezwa, tembelea bit.ly/vaccines26

### Je, huduma gani zinapatikana kwa wakazi wa Jiji la New York?

- NYC Care inaunganisha wakazi wa Jiji la New York—bila kujali mapato wala hali ya uhamiaji—na huduma zinazopatikana kupitia mfumo wa afya ya umma wa Jiji, Health+Hospitals.
- NYC Care haiulizi maswali kuhusu hali ya uhamiaji.
- Unakidhi vigezo vya NYC Care ikiwa wewe:
    - Unakaa katika Jiji la New York
    - Huna bima ya afya kupitia mwajiri wako
    - Hujakidhi vigezo vya mpango wowote wa bima ya afya unaopatikana katika Jimbo la New York
    - Hustahiliki bima ya afya kwa mujibu wa miongozo ya serikali
- Jinsi ya kutuma maombi:
    - Tuma maombi kupitia simu: Piga 646-692-2273
    - Tuma maombi ana kwa ana:
        - Tembelea sehemu ya NYC Health + Hospitals
        - Tembelea shirika la kijamii
        - Tembelea ofisi ya MetroPlusHealth
- Kwa taarifa zaidi, temblea nyccare.nyc

### Rasilimali

**Find a federally qualified health center:**

**NYS Cancer Services:**

**NYS Vaccines:**

**NYC Cares:**

# Afya

## Fahamu Haki Zako katika huduma za afya

### Je, maafisa wa ICE wanaweza kufanya utekelezaji au kumkamata mtu katika kituo cha afya?

- Januari 2025, utawala wa Trump ulifuta sera ya siku nyingi iliyowaelekeza maafisa wa ICE na CBP waepuke kufanya utekelezaji wa uhamiaji katika "mahali maalumu" au "mahali panapolindwa", mfano vituo vya afya. Hii inamaanisha kwamba maafisa wa ICE wanaweza sasa kuingia sehemu za vituo vya afya wanaporuhusiwa kuwepo watu wa umma.
- Hata hivyo, Rekebisho la Nne la Katiba ya Marekani linalinda haki za faragha za watu wote, bila kujali hali zao za uhamiaji. Vituo vingi vya afya vina sehemu za faragha zinazolindwa kutoka utekelezaji wa uhamiaji, isipokuwa maafisa wana hati ya mahakama.

### Je, Jimbo la New York lina ulinzi wowote unaozuia maafisa wa ICE wasiingie vituo vya afya na kuwakamata watu humo ndani?

- Wakazi wote wa New York wana ulinzi kiasi fulani ndani ya vituo vya afya.
- Amri ya Mtendaji wa Jimbo la New York ya 2018 inakataza utekelezaji wa uhamiaji katika majengo ya jimbo la New York kama hospitali, isipokuwa maafisa wa ICE wana hati ya mahakama.
- Mei 27, 2026, Gavana Hochul na Bunge la Jimbo la New York walipitisha sheria mpya inayoitwa Sheria ya Ulinzi wa Mahali Maalumu (Sensitive Location Projection Act), inayowezesha "mahali maalumu" kama hospitali iwakataze maafisa wa utekelezaji wa uhamiaji wasiingie bila ya hati ya mahakama.

### Je, sehemu gani za kituo cha afya zinafikiriwa kuwa "maeneo ya faragha"?

- Vyombo vya utekelezaji wa sheria, zikiwemo ICE na CBP, haviwezi kufanya upekuzi katika sehemu zinazofikiriwa na kutarajiwa kuwa faragha.
- Kila mahali ni tofauti kidogo, lakini inatarajiwa kwamba ofisi za madaktari na vyumba vya kufanyiwa uchunguzi wa kitabibu zifikiriwe kuwa "maeneo ya faragha."
- Sehemu kama chumba cha mapokezi ambazo ni wazi na watu wa umma wanaweza kuingia hazifikiriwi kuwa "faragha," na kwa sababu hiyo hazina ulinzi sawasawa na maeneo ya faragha.

### Je, wagonjwa na wateja wanaweza kufanya nini ili wajilinde? Hospitali zinaweza kufanya nini ili ziwalinde wagonjwa wao?

- Ili kujilinda, wagonjwa wanaweza:
  - Kumwuliza rafiki au mwanajamii aambatane nawe wakati wa kwenda na kurudi kutoka miadi zako
  - Kufahamu haki zako, na kufahamu maeneo gani ni ya faragha na yapi ni ya umma
  - Kufanya mpango na kuwa tayari ikiwa unakutana na maafisa wa ICE au CBP
- Ili kuwalinda wagonja na wateja wao, vituo vya afya vinaweza:
  - Kuonesha na kutambulisha dhahiri maeneo ya faragha
  - Kuwa na itifaki nzuri inayoeleweka kuhusu kufanya nini ikiwa wanakutana na maafisa wa utekelezaji wa sheria, wakiwemo maafisa wa ICE na CBP
  - Kuwapa watumishi wote mafunzo juu ya haki zao na majukumu yao.
  - Kubandika taarifa za Fahamu Haki Zako katika lugha mbalimbali katika sehemu zote za vituo vya afya
  - Kukumbuka ulinzi wa faragha uliopo na kutokuwashirikisha maafisa wa utekelezaji wa sheria taarifa yoyote zaidi kuliko inavyohitajika
  - Kwa taarifa zaidi na mapendekezo, tembelea aclu.org/documents/immigration-enforcement-guidance-for-health-centers

**Rasilimali**

**ACLU's "Immigration Enforcement Guidance for Health Centers"**

# Shule na elimu

## Pata elimu

### Nani anastahilika kuhudhuria shule za umma za Jimbo la New York? Je, ninahitaji kuwa na hali fulani ya uhamiaji?

- Jimbo la New York linahakikisha kuwa kila mtoto, bila kujali hali ya uhamiaji, ana haki ya elimu bure na yenye ubora, kuanzia elimu ya awali hadi aidha anapopokea shahada ya shule ya sekondari, au kufikia kikomo cha umri katika mwisho wa mwaka wa shule ambao mwanafunzi atatimia miaka 21.
- Shule za umma haziwezi kuulizia hali ya uhamiaji na hazitatoa taarifa za wanafunzi kwa programu yoyote ya shule ya kutwa (day school). Baadhi ya programu za watoto wadogo, zinazoendeshwa kwa masaa mengi kuliko kawaida, zinaweza kuweka kigezo cha uraia au kuangalia ukubwa wa mapato.

### Je, vipi najiandikisha katika shule ya umma?

- Wanafunzi wanaweza kutuma maombi na kujiandikisha kwenye shule za umma za Jimbo la New York wakati wowote ndani ya mwaka, ila machaguo yanaweza kuwa machache nje ya kipindi cha kawaida cha kujiandikisha.
- Taarifa za Shule za Umma za Jiji la New York
  - Kwa taarifa kuhusu mchakato wa ruhusa ya kuingia, tembelea schools.nyc.gov/enrollment/enrollment-help/new-students.
  - Kutafuta Shule ya Umma ya Jiji la New York na kutuma maombi ya udahili, piga 311, au tembelea Kituo cha Kukaribisha Familia (Family Welcome Center) kwa msaada. Mahali pa Vituo vya Kukaribisha Familia panapatikana katika schools.nyc.gov/fwc.
  - Vipindi cha kujiandikisha vinatofautiana kutegemea darasa/kidato. Kuona Ratiba ya Udahili kwa Msimu wa Fall 2024 (Fall 2024 Admissions Timeline), tembelea schools.nyc.gov/enroll.

### Je, shule zinaweza kuhitaji kuona hati gani wakati wa kujiandikisha?

- Inawezekana kwamba shule zitawauliza wanafunzi na wazazi kwa ushahidi kwamba mwanafunzi akae katika wilaya ya shule inayohusika. Mifano ya ushahidi huo ni mkataba wa kupangisha nyumba, bili za umeme, fomu za kodi ya mapato, au kitambulisho.
- Inawezekana pia kwamba shule fulani zitahitaji kuona ushahidi kwamba mtu mzima anayemwandikisha mwanafunzi ni mzazi wake au mlezi wake wa kisheria..
- Hata hivyo, shule za umma za Jimbo la New York haziwezi kulazimisha wanafunzi au wazazi wao kutoa namba ya usalama wa kijamii (Social Security number) au taarifa zingine ambazo ni shida kwa watu wasio raia, wanafunzi wasio na vibali, au watu wanaopanga nyumba bila mkataba wa kupangisha nyumba.

### Kuna aina gani za elimu kwa wanafunzi ambao ni watu wazima?

- Katika Jimbo la New York, unaweza kuhudhuria shule za umma hadi utimize miaka 21 au hadi upokee diploma ya shule sekondari.
- Vilevile njia zipo kwa wanafunzi ambao ni watu wazima wanaotaka kujifunza Kiingereza au kupata GED (diploma ambayo ni sawasawa na diploma ya shule sekondari).
- Kutafuta programu ya elimu kwa watu wazima ya hapo karibu ulipo, tembelea acces.nysed.gov/aepp/find-adult-education-program

#### Rasilimali

**NYC Public Schools Enrollment Information:**

**NYS Adult Education Programs:**

# Shule na elimu

## Pata elimu

### Je, wanafunzi na wazazi wanaweza kufanya nini ikiwa haki zao za kupata elimu zinavunjwa?

- Ikiwa unafikiri kwamba shule au wilaya ya shule inajaribu kumfanya mwanafunzi asijiandikishe kwa sababu ya hali yake ya uhamiaji, unaweza kufaili malalamiko kwa Mwanasheria Mkuu wa Jimbo la New York.
- Kwa taarifa zaidi na kujipatia fomu ya malalamiko, tembelea nysed.gov/data-privacy-security/parents-and-students-file-privacy-complaint

### Je, shule za umma zinatoa huduma za tafsiri na ukalimani?

- Familia ndiyo zina haki ya kufanyiwa tafsiri na ukalimani wa nyaraka zote zinazohusika na mambo muhimu ya elimu ya mtoto wao, bila ya kucheleweshwa.
- Kwa taarifa zaidi kuhusu jinsi ya kuulizia huduma za tafsiri na ukalimani katika shule ya umma ya Jiji la New York, tembelea schools.nyc.gov/hello au piga simu 718-935-2013 au 311.

### Je, msaada wa kifedha unapatikana kwa ajili ya kupunguza gharama za chuo/ chuo kikuu?

- Ndiyo, zipo programu kadhaa za msaada wa kifedha za Jimbo la New York.
- Msaada wa kulipa ada (TAP) unawasaidia wakazi wa New York wanaokidhi vigezo kulipa ada katika shule zilizoidhinishwa katika jimbo la New York.
  - Kwa mwaka, msaada wa TAP unaweza kufikia $5,665. Kwa kuwa TAP ni ruzuku, si lazima kuirudisha.
  - Kwa taarifa zaidi au ili kutuma maombi, tembelea hesc.ny.gov/tap
- Udhamini wa Excelsior
  - Udhamini wa Excelsior, pamoja na programu zingine za msaada wa kifedha kwa wanafunzi, unawaweesha wanafunzi kusoma vyuo vya SUNY au CUNY bila kulipa ada.
  - Wanafunzi ambao familia zao zina mapato ya mwaka ya $125,000 au chini ya hapo wanakidhi kigezo cha kutuma maombi.
  - Kwa taarifa zaidi au kutuma maombi, tembelea hesc.ny.gov/excelsior
- Sheria ya DREAM ya Seneta José Peralta ya Jimbo la New York inawapa wanafunzi wasio na vibali vya makazi pamoja na wanafunzi wengine, fursa ya kupata ruzuku zinazotolewa na NYS au ufadhili wa masomo kwa ajili ya kulipia gharama za elimu ya juu.
  - Kwa taarifa zaidi au kutuma maombi, tembelea hesc.ny.gov/dream

### Rasilimali

**NYSED Complaint Form:**

**NYC Schools Interpretation/ Translation Information:**

**Tuition Assistance Program Info:**

**Excelsior Scholarship Info:**

**DREAM Act Scholarship Info:**

# Shule na elimu

## Fahamu Haki Zako katika shule

### Maafisa wa ICE wanaweza kufanya utekelezaji au kumkamata mtu katika shule ya umma ya Jimbo la New York?

- Januari 2025, utawala wa Trump ulifuta sera ya siku nyingi iliyowaelekeza maafisa wa ICE na CBP waepuke kufanya utekelezaji wa uhamiaji katika "mahali maalumu" au "mahali panapolindwa" kama shule.
- Hata hivyo, Rekebisho la Nne la Katiba ya Marekani linalinda haki za faragha za watu wote, bila kujali hali zao za uhamiaji. Maafisa wa ICE na vyombo vingine vya sheria hawawezi kuingia "maeneo ya faragha" bila ya hati ya mahakama au ruhusa kutoka mmiliki. Shule nyingi zina sehemu za faragha zinazolindwa kutoka utekelezaji wa uhamiaji, isipokuwa maafisa wana hati ya mahakama.

### Je, Jimbo la New York lina ulinzi wowote unaozuia maafisa wa ICE wasiingie shule na kuwakamata watu humo ndani?

- Wakazi wa New York wana ulinzi kiasi fulani ndani ya vituo vya afya.
- Amri ya Mtendaji wa Jimbo la New York ya 2018 inakataza utekelezaji wa uhamiaji katika majengo ya jimbo la New York kama shule, isipokuwa afisa wa ICE ana hati ya mahakama.
- Mei 27, 2026, Gavana Hochul na Bunge la Jimbo la New York walipitisha sheria mpya inayoitwa Sheria ya Ulinzi wa Mahali Maalumu (Sensitive Location Projection Act), inayowezesha "mahali maalumu" kama shule iwakataze maafisa wa utekelezaji wa uhamiaji wasiingie bila ya hati ya mahakama.

### Maafisa wa ICE wanaweza kumkamata mwanafunzi akiwa anaenda shuleni au kurudi nyumbani kutoka shuleni?

- Maafisa wa ICE wanaweza, wakati fulani, kuwakamata watu katika sehemu za umma, ikiwemo mitaa ya umma wanafunzi wanapotembea wakati wa kwenda au kurudi kutoka shuleni. Kwenda/ kurudi kutoka shuleni kunaweza kuwa na hatari zaidi kwa sababu wanafunzi wanatembea, kusimama katika vituo vya mabasi, na kusafiri katika magari binafsi.
- Jimbo la New York ndilo lina ulinzi wa maalumu unaowazuia maafisa wa ICE wasiingie mabasi ya shule bila ya hati ya mahakama.

### Je, vipi wanafunzi wanaweza kujilinda? Shule zinaweza kufanya nini ili wanafunzi wao wabaki salama?

- Kujilinda, wanafunzi anaweza:
  - Kumwuliza rafiki au mwanajamii kuambatana nawe wakati wa kwenda na kurudi kutoka shuleni
  - Fahamu hako zako
  - Kufanya mpango na kuwa tayari ikiwa unakutana na maafisa wa ICE au CBP
- Kuwasaidia wanafunzi wao ili wabaki salama, shule zinaweza:
  - Kuonesha na kutambulisha dhahiri maeneo ya faragha
  - Kuwa na itifaki nzuri inayoeleweka kuhusu kufanya nini ikiwa wanakutana na maafisa wa utekelezaji wa sheria, wakiwemo maafisa wa ICE na CBP
  - Kuwapa watumishi wote mafunzo juu ya haki zao na majukumu yao.
  - Kubandika taarifa za Fahamu Haki Zako katika lugha mbalimbali
  - Kukumbuka ulinzi wa faragha uliopo na kutokuwashirikisha maafisa wa utekelezaji wa sheria taarifa yoyote zaidi kuliko inavyohitajika.
  - Kwa taarifa zaidi, tembelea aclu.org/documents/immigration-enforcement-guidance-for-schools

**Rasilimali**

**ACLU's "Immigration Enforcement Guidance for Schools"**

# Usalama wa Jamii



**Kila mtu, bila kujali utambulisho wake au iwapo ana vibali vya makazi au la, anastahili kuwa salama kwenye jamii yake.**

### Ubaguzi na Uhalifu unaotokana na chuki

- Uhalifu wa chuki ni kosa linalosukumwa na ubaguzi kwa sababu ya uasili, rangi, utaifa, jadi, jinsia, dini, imani, umri, ulemavu au mweleko wa kijinsi.
- Jimbo la New York lina Tume Maalumu ya Kudhibiti Uhalifu wa Chuki ili kukabiliana na ongezeko la matukio yanayoripotiwa ya matishio yanayosukumwa na ubaguzi, unyanyasaji na vurugu.
- Ukishuhudia tukio au ikiwa wewe ni mhanga wa uhalifu wa chuki:
  - Toa taarifa kwa Divisheni ya Haki za Binadamu NYS. Piga simu 1-888-392-3644, tuma ujumbe mfupi "HATE" kwenda 81336, au tembelea forms.ny.gov/s3/Hate-Crime-Tips. Tembelea dhr.ny.gov kwa taarifa zaidi.
  - Kuripoti uhalifu wa chuki ukiwa unatokea au hali yoyote ya hatari, piga 911 haraka.
- Uhalifu wa chuki ukiripotiwa, taarifa zote kuhusu uliyopitia, utambulisho wako na wa wengine unabaki kuwa siri.
- Unaweza kutoa taarifa kuhusu uhalifu wa chuki na kupewa huduma bila kujali iwapo una vibali vya makazi au la.

### Rasilimali za Kijamii

- Ofisi ya Kuzuia Uhalifu wa Chuki ya Jiji la New York inatoa huduma, taarifa , na msaada kwa wanajamii na mashirika mbalimbali. Taarifa zinapatikana katika lugha mbalimbali. Kwa taarifa zaidi, tembelea nyc.gov/stophate
- Kituo cha Kutoa Elimu ya Kuzuia na Kupambana na Vurugu kinafanya kazi ya kuzuia, kupambana na kuponya jamii ya New York na uhalifu wa chuki. Wana programu za elimu ya kujilinda, warsha zinazowalenga washuhudiaji, na kuwawezesha vijana. Piga 1-718-788-1775 au tembelea caeny.org kwa taarifa zaidi.

### Mitandao ya Kijamii Unayoweza kujiunga

- AAPI
  - Asian Americans for Equality: 212-979-8381, aafe.org
  - Chhaya for South-Asian and Indo-Caribbean communities: 718-478-3848, chhayacdc.org
  - Korean Family Service Center: 718-460-3800, kafsc.org
  - MinKwon Center for Community Action: 718-460-5600, minkwon.org
  - National Federation of Filipino American Associations New York: 212-684-0542, naffaa.org
  - Sikh Coalition: 516-930-0302, sikhcoalition.org
- Waafrica
  - African Communities Together: 347-746-2281, africans.us
  - African Services Committee: 212-222-3882, africanservices.org
  - Sauti Yetu Center For African Women: 718-665-2486, sautiyetu.us
- Waarabu/Waislamu
  - Arab American Association of New York: 718-745-3523, arabamericanny.org
  - Council on American-Islamic Relations of New York: 646-665-7599, cair-ny.org
  - Muslim Community Network: 347-519-2755, mcnny.org
- Watu wenye ulemavu
  - Center for Disability Rights: 585-546-7510, cdrnys.org
  - Disability Rights New York: 518-432-7861, drny.org
- Hispanic/Latino
  - Hispanic Federation: 866-432-9832, hispanicfederation.org
  - Latino Commission on AIDS: 212-584-9325, latinoaids.org
  - Mixteca: 718-965-4795, mixteca.org
  - TransLatinx: 646-882-2000, translatinxnetwork.org
- LGBTQ+
  - Caribbean Equality Project: 347-709-3179, caribbeanequalityproject.org
  - Gay, Lesbian, Bisexual and Transgender Community Center: 212-620-7310, gaycenter.org
  - New York City Gay and Lesbian Anti-Violence Project: 212-714-1141, avp.org
- Native American na Alaska Native
  - American Indian Community House: 646-575-3638, aich.org
  - North American Indigenous Center of New York: 516-930-0302, naicny.org

# Taarifa zinazopatikana NYS



**Ofisi ya Upatikanaji wa Lugha ya NYS (Jimbo la New York)**

- Ofisi ya Upatikanaji wa Lugha ya NYS inasimamia upatikanaji wa huduma za lugha kwa mamilioni ya wakazi wa New York wasio na ustadi kamili wa lugha ya Kiingereza.
- Kufahamu haki zako za kupata huduma za ukalimani na tafsiri, tembelea ogs.ny.gov/know-your-rights
- Kufaili malalamiko kuhusu upatikanaji wa lugha, tembelea languageaccess.ny.gov/en-US.
- Kupokea toolkit (mkusanyiko wa zana) ya upatikanaji wa lugha, au kuomba toolkit ya ukalimani, uwasilishe hojani kwa mashirika ya utetezi survey.alchemer.com/s3/8252338/OLA-Questionnaire

**NYS Ofisi ya Wamarekani Wapya**

- Ikiwa wewe au mtu unayemfahamu anahitaji msaada wa bure wa kisheria, piga simu ya bure 1-800-566-7636. Taarifa zote zitatunzwa kwa usiri. Msaada unatolewa kwa zaidi ya lugha 200.

**NYS Kitengo cha Afya**

- Tuma maombi ya bima ya afya: piga 1-855-355-5777 au tembelea nystateofhealth.ny.gov.

**NYS Ofisi ya Afya ya Akili**

- Kwa taarifa zaidi kuhusu huduma za matibabu ya afya ya akili au kupata mhudumu wa matibabu ya afya ya akili, piga 1-800-597-8481 au tembelea omh.ny.gov.
- Huduma ya Kitaifa ya Kuzuia Kujiua: Ikiwa maisha yako au ya mtu unayemfahamu yako hatarini, piga 911. Ikiwa uko hali ya hatari au unahitaji msaada wa haraka, piga 1-800-273-8255 au tuma SMS "GOT5" kwenda 741-741.

**NYS Ofisi ya Kuzuia Unyanyasaji wa Kijinsia**

- Iwapo wewe au mtu mwingine aliye katika mahusiano ananyanyaswa na mtu mwingine kwa maneno, vitendo au kingono, au unyanyasaji wa aina nyingine, piga simu ya bure Ofisi ya NYS inayoshughulikia Unyanyasaji wa Kijinsia 1-800-942-6906.
- Kuzungumza na mshauri kwa njia ya mtandao, tembelea opdv.ny.gov. Inapatikana 24/7 katika lugha mbalimbali.

**NYS Kitengo cha Kazi**

- Kitengo cha Kazi kimejikita katika kulinda usalama wa wafanyakazi pamoja na afya, malipo/mishahara na mazingira mazuri za kazi.
- Kwa taarifa kuhusu sheria zinazohusu maslahi na masaa ya kazi, afya na usalama wa wafanyakazi, au kutuma malalamiko, piga 1-888-469-7365 au tembelea dol.ny.gov/safety-and-health
- Kwa msaada wa Bima ya Kukosa Ajira, piga 1-888-209-8124 au tembelea dol.ny.gov/unemployment/unemployment-insurance-assistance.

**NYS Kitengo cha Haki za Binadamu**

- Sheria ya Haki za Binadamu ya New York inakataza ubaguzi katika ajira, makazi, mikopo, elimu, na haki ya kuwepo sehemu za umma, kwa sababu ya umri, uasili, utaifa, jinsia, mwelekeo wa kijinsi, jinsi, ndoa, ulemavu, uanajeshi, na kadhalika.
- Ikiwa unahisi umebaguliwa, tuma malalamiko 1-888-392-3644 au tembelea dhr.ny.gov.

**NYS Makazi**

- Kwa msaada wa kutafuta makazi ya bei nafuu, piga 1-877-428-8844 au tembelea nyhousingsearch.gov.
- Kwa taarifa ya jinsi ya kushiriki kwenye bahati nasibu ya kupata makazi kwa bei nafuu katika jiji la New York, piga 212-863-7990 or visit housingconnect.nyc.gov.
- Kwa taarifa kuhusu haki za wapangaji kwenye Jimbo la New York, tembelea ag.ny.gov/publications/residential-tenants-rights-guide.

**Ofisi ya Huduma za Wahanga ya NYS**

- Iwapo wewe au mtu unayemfahamu ni mhanga wa uhalifu wa chuki, Ofisi ya Huduma za Wahanga ya NYS inaweza kusaidia kulipa gharama za huduma za matibabu na ushauri nasaha, malipo yaliyopotea, na msaada wa aina nyingine.
- Piga 1-800-247-8035 au tembelea ovs.ny.gov kwa taarifa zaidi.

Kusoma taarifa hii mtandaoni au kwa lugha nyingine, tembelea nyic.org/KYR or skani kodi hii:

Iwapo una swali lolote au maoni kuhusu nyenzo au taarifa ndani yake, tafadhali wasiliana na:
Bryan Lee – blee@nyic.org

Shirikisho la Wahamiaji wa New York (NYIC) ni sera jumuishi na shirika la utetezi linalowakilisha zaidi ya makundi 200 yanayotetea haki za wahamiaji na wakimbizi waliopo New York.

Tunaiona New York iliyo imara zaidi kwa sababu watu wote wanakaribishwa, wanahudumiwa kwa usawa na wanapewa nafasi ya kufikia ndoto zao. Dhima yetu ni kuwaunganisha wahamiaji, wanajamii na wadau ili wakazi wote wa New York wote waweze kustawi.

NYIC

**New York Immigration Coalition**
131 W 33rd St, Ste 610
New York, NY 10001
212 627 2227
nyic.org